JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA KUMI NA MOJA

Novemba 2023



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA

# Majaliwa asisitiza nidhamu, maadili, ubunifu kwa watumishi wa umma

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amewataka watumishi wa umma wafanye kazi kwa bidii, weledi, nidhamu, uadilifu na ubunifu ili kutimiza maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

Amesema kila mtumishi anapaswa kutambua kuwa mafanikio katika utekelezaji wa majukumu, mipango na mikakati wanayoisimamia yanahitaji juhudi ya kila mtumishi na nidhamu katika kufanya kazi.

Ametoa wito huo katika kikao na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake katika ukumbi wa mikutano wa PSSSF jijini Dodoma.

"Nitoe wito kwa kila mtumishi kuzingatia nidhamu ya kazi na maadili ya utumishi wa umma, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inatekeleza falsafa ya Kazi Iendelee. Kwa msingi huo watumishi wote wa umma mnao wajibu wa kufuata na kutekeleza falsafa hii. "

Aidha, Mheshimiwa Majaliwa amewapongeza watumishi hao kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao vizuri na kwa weledi. "Kujituma kwenu, ushirikiano na bidii vimewezesha Serikali na hususan Ofisi ya Waziri Mkuu kupata mafanikio makubwa. "

Katika hatua nyingine, Mheshimiwa Majaliwa amesema kuwa tangu Rais Dkt. Samia aingie madarakani amekuwa anatoa msukumo wa kuboresha mazingira ya watumishi na kusisitiza kushughulikia stahiki mbalimbali za watumishi wa umma ikiwemo ulipaji wa malimbikizo ya mishahara, upandishaji wa madaraja na utoaji wa ajira mpya.

"Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amelipa madai malimbikizo ya mishahara ya watumishi 121,858 yenye jumla ya shilingi bilioni 207.97, pia amepandisha madaraja watumishi 91,841 na shilingi bilioni 73.4 zimetumika kuwalipa watumishi hao"



Pia, Mheshimiwa Majaliwa aliwakumbusha watumishi hao kusimamia kikamilifu na kwa makini miradi na programu zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili Ofisi isipoteze fursa ya kuungwa mkono na Taasisi za Kimataifa "Endeleeni kutoa huduma bora za Serikali kwa umma pamoja na kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali katika sekta zote kwa ufanisi na tija. "

Akizungumza katika kikao hicho, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko amewashukuru watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wanaoendelea kumpa katika majukumu yake ya kila siku.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Jenista Mhagama amesema kuwa wataendelea kusimamia mipango ya kitaifa na ya kisekta kwa uaminifu mkubwa ili kuleta matokeo chanya Serikalini

Naye, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Prof. Joyce Ndalichako amewataka watumishi hao kufanya kazi kwa umoja na mshikamano ili waweze kufanikiwa kutekeleza ipasavyo majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ufanisi wa hali ya juu.

.

# Waziri Mhagama Aagiza kuimarishwa miundombinu ya mawasiliano Dar



Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI imeahidi kutoa kiasi cha shilingi Milllioni 20 ili kuimarisha kivuko cha kivuko cha Magole/Mwanagati kilichopo katika kata ya Mzinga Halmashauri ya Ilala Mkoani Dar es salaam ili kiweze kupitika muda wote.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe, Jenista Mhagama wakati akizungumza na wakazi waliojitokeza katika eneo hilo la kivuko liloathirika na Mvua.

wakati wa ziara yake iliyolenga kupata taarifa zilizochukuliwa na Kamati ya Mkoa ya Maafa juu ya kudhibiti madhara ya zaidi mvua yanayoweza kujitokeza.

Ameongeza kusema kazi ya kuimarisha kivuko ifanywe na wakala wa barabara vijijini TARURA haraka iwezekanavyo.

“Kivuko hiki kitakapokuwa kinapitika muda wote hakitarudisha juhudi ya kwenda na Mpango wa pili wa muda mrefu wa kujenga daraja la kudumu,”alibainisha

Waziri mhagama alisema kuwa serikali inatamani kuona shughuli za wananchi zifanyika bila kusimama; tunatamani watoto wetu waende shule, tunatamani kina mama wajawazito waende kupata huduma za afya kwa wakati, tunapenda wananchi wajisikie serikali yao inawajali, alisema Waziri.

"Tunataka tutengeneze daraja livutie machoni pa watu, kile matumaini kwa watu kwamba hii ni nyota ya Mhe. Rais, Dkt, Samia Suluhu Hassan na wananchi washirikishwe kiasi cha kutosha," alifafanua

Waziri Mhagama alielekezaTARURA kuifanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa na kwa hofu ya mungu, kwa sababu mnasimamia uhai na maisha ya watu na sisi tunawaamini na tunawategemea.

Katika hatua nyingine Waziri ameomba wananchi kuendelea kuchukua tahadhari juu ya magonjwa ya mlipuko; hali ya mvua inaweza kutupelekea kwenye magonjwa ya kuhara, magonjwa ya malaria.

Aliwaasa wananchi kuendelea kusafisa vichaka na kujenga utaratibu mzuri wa kusafisha mazingira yetu na kila mmoja awe askari wa mwenzake na kuhakikisha mifereji yetu inakuwa safi na mapito ya maji yanakuwa wazi.

Kwa upande Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Mhe. Albert Chalamila alisema Mkoa wa Dar es salaam umeathiriwa na wa ujenzi wa kutawanyika, hivyo kasi ya ujenzi wa miundombinu imekuwa gharama kubwa, lakini lazima hilo lifanyike kwa sababu ni huduma kwa watanzania.

Wataalamu wetu wamekuwa wakisanifu ramani za daraja lakini bado hatujapata fungu la fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja, na hapa tunahitaji mkakakati mkubwa wa kuzuia mto kutokula kingo zake.

:Tunajitahidi kuhakikisha wananchi hawajengi mabondeni; na kulinda mito dhidi ya shughuli za kibinadamu, ikiwa ni sambamba na kuhakikisha tunaunganisha miundo mbinu ya mawasiliano ili mambo yaweze kwenda vizuri," alifafanua Mkuu wa Mkoa.




Serikali kuongeza nguvu mapambano ya VVU kwa kundi la vijana.

Imeelezwa kuwa kundi la vijana kati ya umri wa miaka 15 mpaka 24 wanaongoza kwa kuchangia maambikizi mapya ya VVU – UKIMWI ambayo ni sawa na Asilimia 40 (40%).

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama ameyasema hayo mapema leo Ofisini kwake Jijini Dodoma alipokuwa katika Mkutano na waandishi wa Habari uliyohusu maandalizi ya kilele cha maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani, yanayofanyika Disemba moja kila mwaka.

Akiongelea kuhusu maadhimisho hayo yanayotarajiwa kafanyika kitaifa Mkoani Morogoro mwaka huu, Waziri Mhagama alisema tafiti zilizopo zinaonesha kuwa kuna kila sababu ya kuongeza nguvu kubwa kwa kundi la vijana ili kuliondoa kwenye uhatarishi wa maambukizi ya vvu.

Aliendelea kusema kuwa maadhimisho ya mwaka huu yatatoa kipaombele kwa kiasi cha cha kutosha kwa vijana kushiriki kikamilifu kwenye majukwaa na matukio

yaliyoandaliwa kwenye maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani mwaka huu nchini kote kutokana na sababu kwamba vijana ndo waingia kwenye maambukizi mapya kwa wingi.

"Tunapokwenda huko mbele walau kwenye maadhimisho ya wiki ya kuelekea siku ya UKIMWI Duniani, tutoe nafasi ya kuwasikiliza vijana kwa karibu zaidi wakongamane, wakutane na viongozi wa dini na viongozi wa kimila, na wakati mwingine tumekuwa tukifikiri kwamba labda, mienendo ya kimaadili kwa sasa imekuwa ikichagiza vijana wetu kujikuta wanaingia kwenye kundi la maambukizi mapya kwa hivyo kwa kipindi hiki kipaombele kitakuwa kwa kundi la vijana." Alifafanua Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama alisema kuwa zaidi ya mara tano tafiti zinaonesha kuwa wanawake wamekuwa na uhiyari wa kupima ukilinganisha na wanaume; ambao hawajitokezi kupima na kuanza matumizi ya dawa, hivyo kuna kila haja ya Serikali kupaza sauti juu kuwaomba kina baba waingiwe na hali ya uhiyari katika kufanya maamuzi ya kupima.

Kwa Upande wake Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU (NACOPHA) Bw. Emmanuel Reuben Msinga alisema kuwa kupitia Kliniki ya Huduma na Kinga (CTC) vijana wanaweza kufikiwa kwa wingi na kupata hamasa ya kupima kwa hiyari, na vijana wanahamasishana kukubali hali zao na namna ya kuwafikia vijana wingine ili wakapime kwa hiayari.

Aliongeza kusema kuwa NACOPHA ina kanda zake nchini na suala la uhamasishaji kwa sasa linafanyika kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya na Mikoa.

Kauli Mbiu kwa Maadhisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kwa mwaka huu inasema; "JAMII IONGOZE KUTOKOMZEA UKIMWI."



SASA Yapongezwa upatikanaji wa mbegu bora za kilimo.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Ummy Nderiananga ameupongeza Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) kwa kukamilisha Awamu ya Kwanza ya Mradi wa miundombinu ya Umwagiliaji katika shamba la mbegu Kilimi lililopo Wilaya ya Nzega mkoani Tabora.

Mhe. Ummy ameyasema hayo wakati wa ziara yake ya kikazi katika shamba la mbegu Kilimi linalotekelezwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) kupitia Mradi wa Kuendeleza Kilimo Kilimo na Uvuvi (AFDP) unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu ambapo amesema Taasisi hiyo iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo imepiga hatua kwa utekelezaji wa vitendo kwa ujenzi wa miundombinu ya kisasa na imara ya Umwagiliaji katika shamba hilo.

Amesema matarajio ya Serikali ni kuona uzalishaji wa mbegu unaongezeka kwa wananchi ili kupunguza uagizwaji wa mbegu kutoka Nchi jirani

ambapo baadhi ya wakulima hushindwa kumudu gharama.

"Namshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha tufanya kilimo cha kisasa na kupata fedha za kuendeleza sekta hii muhimu lengo la ziara hii ni kuona Mradi unavyoendelea hivyo nampongeza Waziri wa Kilimo Mhe. Bashe anafanya kazi kubwa sana akishirikiana na ASA. Pia nimefurahi kuona fedha inayokuja katika mradi inafanya kazi iliyokusudiwa kuongeza tija katika uzalishaji wa mbegu,"Alisema Mhe. Ummy.

Ameeleza kwamba Wizara ya Kilimo imejipambanua kwa kuweka miundombinu ya Umwagiliaji, kuhamasisha vijana kukipenda kilimo tofauti na awali kilichukuliwa kama adhabu.

"Tunawashauri watanzania waendelee kuiamini Serikali wakati tunafanya mapinduzi ya kilimo watumie fursa hii hasa waliopo katika maeneo haya na hata tutakapoanzisha vituo hivi katika maneno mengine basi wakulima watumie fursa hiyo kuboresha kilimo wajikwamue kiuchumi,"Ameeleza.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) Dkt. Sophia Kashenge amesema maelekezo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri yatafanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa mbegu ili kukidhi mahitaji ya wakulima hapa Nchini huku akisema kuwa wataendelea kuweka mikakati ya kuimairisha usalama katika mashamba kuepuka uharibifu unaotokana na uingizwaji wa mifugo katika mashamba hayo.

"Awali kulikuwa na changamoto kubwa ya mifugo kuingia katika mashamba lakini tumejitajidi kutoa elimu kwa vijiji vilivyopo katika maeneo haya na tunaendelea kuongeza ulinzi kimsingi mifugo ina madhara makubwa kwa mashamba ya mbegu na uzalishaji wa chakula pale mifugo inapoleta magugu kupitia kinyesi, wanaharibu rutuba ya udongo, kuongezeka kwa magonjwa kwa mazao hali inayoongeza gharama za matunzo," Alifafanua Dkt. Sophia.

# Tanzania kuendelea kufanya tathmini ya hiari katika utayari wa kukabiliana na majanga




Imeelezwa kuwa Serikali itaendelea kufanya tathmini ya hiari dhidi ya utayari wake katika kukabiliana na majanga hasa milipuko ya magonjwa hivyo tathmini zitasaidia katika kukabiliana na milipuko hiyo na kuboresha maeneo mbalimbali yanayolinda afya za watu wetu.

Hayo yameelezwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi wakati wa Kikao Kazi cha Makatibu Wakuu Kupitia na Kujadili Rasimu ya Taarifa ya Tathmini ya Hali ya Utekelezaji wa Afya kwa Wote na Utayari wa Kukabiliana na Dharura

kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya TAKWIMU Jijini Dodoma

Dkt. Yonazi alieleza kuwa, upo umuhimu wa kufanya tafiti na tathmini hizo kwa kuzingatia uwepo wa milipuko ya magonjwa mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maeneo mbalimbali yanayolinda afya za watu wetu.

"Leo tumekutana na Makatibu Wakuu na wataalam wetu kuangalia namna ambavyo tathmin iliyofanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo upande wa sheria, mifumo na kuona utayari wetu katika maeneo yote muhimu ikiwemo afya, maji, miundombinu, ili kuhakikisha afya ya mtanzania inalindwa, kwa kuwa jambo hili ni la Kitaifa na tunajilinganisha na mataifa mengine ilikuwa muhimu kufanya tathmini hiyo ili kuona matunda ya matokeo katika kuboresha afua za afya," alieleza Dkt. Yonazi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amesema kuwa Wizara ya Afya imeendelea kujipanga katika kuhakikisha inakabiliana na magonjwa ya milipuko endapo ikitokea.

"Wizara ya Afya itaendelea kuhakikisha huduma za afya zinapatikana sehemu zote nchini, tunaendelea kuhakikisha kunakuwa na vitendea kazi na watenda kazi kwa kuendelea kuajiri watumishi wa kada ya afya na kuwa na utayari na weledi wa kutosha katika kukabili majanga endapo yatatokea," aslisema Dkt. Jingu

Aliongezea kuwa Wizira itaendelea kuajiri watendaji na kuwajengea uwezo kupitia mafunzo mbalimnbali ili kuwa na mbinu za kutosha katika kutoa huduma kwa jamii na kuhakikisha afya za watu wetu zinalindwa.

"Wizara imekuja na mpango wa kuwa na community Health works katika kila kijiji, mtaa hadi mijini ambao watakuwa wanajitolea, sisi tutawawezesha mafunzo na ujuzi katika kuchukua hatua za awali inapotekea suala la maafa." Alisisitiza.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz